

JARIBIO LA MTHANI

DARASA LA TANO - MWAKA 2019

KISWAHILI: LUGHA



002

5

SEHEMU YAKWANZA: LUGHA

SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI

Muda: Saa 1 Dakika 40

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:
 - (i) Jina lako
 - (ii) Jina la shule yako

Kifungu kifuatacho kina nafasi 1 hadi 15. Chagua jibu lililo bora zaidi kujaza pengo.

Siku ___ 1 ___ Ijumaa tarehe tatu mwezi ___ 2 ___ tano. Mwalimu mkuu wa ___ 3 ___ yetu alimwambia kinara wa shule awakusanye wanafunzi ___ 4 ___ nje ya afisi ___ 5 ___.

___ 6 ___ sote tulishangaa ___ 7 ___ si kawaida kukusanyika ___ 8 ___ ya jioni. Tulimsubiri mwalimu mkuu ___ 9 ___ hamu atueleze ___ 10 ___.

“Siku ya Jumamosi ___ 11 ___ siku ya mazingira,” Mwalimu mkuu alianza kueleza, “Idara ya mazingira imealika walimu ___ 12 ___ na wanafunzi wote kutoka darasa la tano hadi la nane ili wapande ___ 13 ___ siku hiyo. Tutaandaliwa ___ 14 ___ cha mchana na tutapatiwa vazi ___ 15 ___ rangi ya kijani kibichi. Mwalimu mkuu alimalizia.

- | | | | | |
|-----|----------------|----------------|---------------|--------------|
| 1. | A. za | B. ya | C. wa | D. cha |
| 2. | A. ya | B. za | C. cha | D. wa |
| 3. | A. idara | B. shule | C. maktaba | D. somo |
| 4. | A. sote | B. lote | C. wote | D. zote |
| 5. | A. yao | B. wao | C. yake | D. zote |
| 6. | A. wao | B. nyingi | C. sisi | D. wale |
| 7. | A. kwani | B. kwa sababu | C. kama vile | D. vile |
| 8. | A. masaa | B. saa | C. muda | D. nyakati |
| 9. | A. wa | B. kwa | C. mwa | D. la |
| 10. | A. alilotuitia | B. yaliyoitiwa | C. walioitiwa | D. tuliloita |
| 11. | A. ndio | B. na | C. ni | D. ndimi |
| 12. | A. mmoja | B. pamoja | C. mbili | D. mkuu |
| 13. | A. miti | B. ngazi | C. madaraka | D. gari |
| 14. | A. vyakula | B. mulo | C. kande | D. chakula |
| 15. | A. za | B. la | C. ya | D. wa |

Kutoka swali la 16 hadi 30, chagua jibu sahihi kujaza pengo.

16. Kitendawili

Huku ng'o kule ng'o?

- A. njaa B. kukosa chochote
C. giza D. sherehe

17. Umbo hili ni



- A. mstatili B. pembe tatu
C. mraba D. tufe

18. Kusikia ni kwa sikio kama vile _____ ni kwa pua.

- A. kulia B. kucheka
C. kiota D. kunusa

19. Makao ya kuku ni

- A. nyumba B. kizimba
C. kiota D. zizi

20. Andika kwa wingi

Mtoto ameanguka uani

- A. watoto wameangukia nyuani
B. Watoto wameanguka mauani
C. Vitoto vimeanguka mauani
D. Matoto yameanguka nyuani

21. Onyango alienda hospitalini akadungwa _____ na daktari

- A. shindano B. dawa
C. machela D. sindano

22. Alama! huitwaje?

- A. kiulizi B. kikomo
C. mshangao D. kituo

23. Shairi la mishororo minne huitwa

- A. tathlitha B. tarbia
C. takhmisa D. mloto

24. Taja akisami hii $\frac{1}{3}$


- A. thuluthi B. subui
C. thumni D. tusui

25. Kamilisha methali

Mtoto umleavyo ndivyo?

- A. akuayo B. akuwaye
C. akuwayo D. akuavyo

26. Taja jina la umbo hili



- A. moyo B. mche
C. kopa D. pia

27. Kitambaa kinachowekwa dirishani huitwa

- A. dari B. shubaka
C. zulia D. pazia

28. _____ hufungwa kichwani na wanaume.

- A. Kidotia B. Kilemba
C. Surupwenye D. Paji

29. Kamilisha tashbihi

Chungu kama _____

- A. shubiri B. pilipili
C. asali D. halua

30. Jiko linalotumia makaa huitwa:

- A. meko B. gesi
C. seredani D. tea

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40

Hapo jadi, paliondokea bibi mmoja kwa jina Jinoking'ang'i. Nyanya huyu aliishi katika kijiji kilichoitwa Mpuku kilichokuwa karibu na msitu ulioitwa Tuatugawe. Ni katika kijiji hiki ambako kulikuwa na wanyama wenye magamba kama vile kasa.

Jinoking'ang'i aliwapenda sana wajukuu wake. Kila usiku kabla ya kulala, alihakikisha amewasimulia hadithi. Nyanya huyu alikuwa mweusi tititi na mguu wake wa kushoto ulikuwa na tenge hivyo basi alitembea kwa mkongojo. Kila jioni alizinga kuni hasa kigongo cha mvule. Alasiri moja alipokuwa kwenye harakati za kugeuza gogo moja, kenge alijitokeza na kupitia kwenye mwanya wa miguu.

"Simile! mburukenge wewe." Nyanya alisema "Yapata miongo mitatu tangu ni mwone mnyama huyu." Baada ya shtusho hilo, Jinoking'ang'i alibeba tita lake kisha akaelekea kiamboni. Kufika nyumbani, aliwasha moto kwenye nje ya nyumba ya msonge iliyokuwa imezekwa kwa nyasi. Wajukuu wa nyanya huyu walimpa sana na hivyo wakampatia kiti chake na akakikalia tayari kusimulia hadithi. "Hadithi, Hadithi!" nyanya alianza, "Hapo zamani za kale....."

- | | |
|--|--|
| <p>31. Kijiji ambacho nyanya alimoishi kilikuwa chaitwaje?
A. Tuatugawe. B. Ngaramba
C. Punkutu D. Mpuku</p> <p>32. Msimulizi wa hadithi alikuwa nani?
A. Shangazi. B. Halati.
C. Nyanya. D. Babu.</p> <p>33. Tunasema mweusi tititi ilhali tunasema mweupe
A. rovurovu B. pepepe
C. sisisi D. tititi</p> <p>34. Jina jingine la nyanya ni
A. bibi B. mama mkwe
C. mkoi D. bikizee</p> <p>35. Msitu uliokuwa karibu na kijiji uliitwaje?
A. Mpuku. B. Msonge.
C. Magamba D. Tuatugawe.</p> | <p>36. Nyumba ya msonge ni nyumba iliyoezekwa na
A. matofali B. saruji
C. nyasi D. mabati</p> <p>37. Mguu uliopindika au uliokombo hukusudiwa kuwa na
A. poza B. tenge
C. nundu D. kiwete</p> <p>38. Neno 'simile' limepigwa mstari maana yake ni kutaka
A. kuapishwa B. apishwe ili apite
C. kushangaa D. heshima yake</p> <p>39. Kipindi cha miaka kumi huitwa
A. mwongo B. karne
C. milenia D. korija</p> <p>40. Twasema bunda la noti, pia tita la
A. mawe B. mikuki
C. nyumba D. kuni</p> |
|--|--|

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50

Ni muhimu tunapokutana na watu kuamkiana nao. Watu wazima tuwaambie shikamoo. Watoto wale ambao ni rika na sisi au marafiki tuwajulie hali zao. Lakini utaona mara nyingi hatufanyi hivyo. Kuamkiana kunaleta furaha na utulivu nyoyoni. Pia tunawajibika kutumia maneno kama sahamahi, póle, nisamehe na niwie radhi. Maneno haya yanaonyesha heshima ya mtu anayetumia.

Anyango, Bahati na Wanyonyi ni wanafunzi wenye heshima sana kwa kuwa hutumia maneno yenye adabu.

41. Ukikutana na mtu mzima unatakikana kumuamkua vipi?
A. Habari. B. Mambo.
C. Shikamoo. D. Sasa.
42. Kuamkiana kuna leta
A. hasira B. furaha
C. huzuni D. nderemo
43. Neno lipi kati ya haya si neno la adabu?
A. Nisamehe. B. Tafadhali.
C. Niwie radhi. D. Mjinga.
44. Mtu mwenye kutumia maneno ya adabu huambiwa ana
A. heshima B. bidii
C. hasira D. shida
45. Habari hii inatufundisha kuwa mtu mwenye kutumia maneno ya adabu ni mtu mwenye tabia
A. njema B. mbaya
C. ya kuhuzunisha D. ya chuki
46. Kwa nini ni vizuri kuamkiana
A. Kunaleta huzuni nyoyoni
B. Kunaleta utulivu nyoyoni
C. Kunaleta subira nyoyoni
D. Kunaleta hasira nyoyoni
47. Ni nini inawafanya Anyango, Bahati na Wanyonyi kuitwa watoto wenye heshima?
A. Michezo wanayocheza
B. Jinsi wanavyoongea.
C. Jinsi wanavyofanya kazi
D. Jinsi wanavyochekeza
48. Kuwa na heshima si
A. kuwa na maneno matamu
B. kuwa na marafiki wengi
C. kuwa na tabia mbaya
D. kuwa na tabia nzuri
49. Wahengo husema heshima si
A. bure B. maneno
C. utumwa D. ulevi
50. Kichwa cha habari kinaweza kuwa
A. Bahati nzuri.
B. Adabu.
C. Maneno mengi.
D. Habari mbaya.

STDS		#	STDS	#	STDS	#	STDS
1	B	46	A	1	B	46	B
2	B	47	C	2	C	47	C
3	A	48	A	3	A	48	B
4	B	49	D	4	A	49	D
5	C	50	A	5	B	50	D
6	D			6	C		
7	B			7	D		
8	C			8	D		
9	B			9	D		
10	B			10	C		
11	A			11	B		
12	B			12	A		
13	B			13	B		
14	C			14	A		
15	C			15	C		
16	D			16	A		
17	D			17	A		
18	B			18	C		
19	D			19	D		
20	B			20	C		
21	C			21	B		
22	A			22	A		
23	B			23	A		
24	C			24	A		
25	C			25	C		
26	C			26	C		
27	D			27	B		
28	A			28	B		
29	D			29	B		
30	B			30	D		
31	A			31	C		
32	C			32	A		
33	A			33	C		
34	B			34	D		
35	A			35	C		
36	B			36	B		
37	A			37	B		
38	D			38	D		
39	A			39	A		
40	B			40	B		
41	A			41	A		
42	A			42	D		
43	C			43	D		
44	B			44	A		
45	B			45	A		
				46	B		

STDS

Marking scheme